# Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Simu: +255 26-2963822
Nukushi: +255 26-2963828
Barua pepe: sg@nbs.go.tz
Tovuti: www.nbs.go.tz

Barabara ya Jakaya Kikwete,
S.L.P. 2683,
Dodoma
**TANZANIA.**


*Unapojibu tafadhali taja:*
Kumb Na: AC 334/376/01/26

**YALIYOJITOKEZA**

Tarehe: 08 Novemba, 2022

## FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA KWA MWEZI OKTOBA, 2022

## 1. MAELEZO YA MBINU NA KANUNI ZA UKOKOTOAJI WA FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA

### 1.1 Maana ya Fahirisi za Bei za Taifa

Fahirisi za Bei za Taifa (FBT) ni kipimo kinachotumika kupima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazotumiwa na sampuli wakilishi ya kaya binafsi nchini Tanzania. Kapu linalotumika kukokotoa FBT lina jumla ya bidhaa 383 ambazo bidhaa 132 ni za Vyakula na Vinywaji Baridi, na bidhaa 251 ni bidhaa zisizo za vyakula. Kwa wigo wa kijiografia, FBT zinakokotolewa kwa kutumia takwimu za bei zinazokusanywa kwenye makao makuu ya mikoa yote 26 ya Tanzania Bara.

### 1.2 Mizania za Fahirisi na Kizio

Mizania za Fahirisi za Bei za Taifa zimetokana na matumizi ya kaya binafsi kwenye ununuzi wa bidhaa na huduma katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara kwa maeneo ya mijini na vijijini. Matokeo ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa Mwaka 2017/18 yalitumika kama chanzo kikuu cha takwimu za uandaaji wa mizania za Fahirisi. Kizio cha Bei cha Fahirisi zilizofanyiwa marejeo kimeboreshwa na kuwa wastani wa bei za mwezi Januari hadi Desemba 2020, na kizio cha Fahirisi ni mwaka 2020.

### 1.3 Makundi ya Bidhaa na Huduma za Jamii

Fahirisi za Bei za Taifa zinatumia mpangilio wa kimataifa wa matumizi binafsi ujulikanao kama COICOP "*Classification of Individual Consumption by Purpose*" wa mwaka 2018. Aidha, Fahirisi za Bei zinatolewa kwenye makundi 13 ya mpangilio wa COICOP, 2018 pamoja na fahirisi za bei kwa makundi maalumu ambayo yanajumuisha: - Fahirisi za msingi (*core index*); Fahirisi ya nishati, mafuta na huduma za maji; Fahirisi isiyo ya msingi *(Noncore index);* Fahirisi ya huduma; Fahirisi ya bidhaa; Fahirisi ya huduma za elimu na bidhaa zinazoambatana nazo na Fahirisi ya bidhaa zote isiyojumuisha bidhaa za vyakula na vinywaji baridi.

### 1.4 Namna ya Kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa

Ukokotoaji wa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi za mwanzo unatumia wastani wa jiometria "*geometric mean of Price Relatives*". Kanuni ya Fahirisi ya *Lowe Index Formula* ambayo ni aina ya "*Laspeyres Index Formula*" hutumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi ya makundi makubwa.

## 2. MFUMUKO WA BEI WA TAIFA KWA KIPIMO CHA MWAKA UMEONGEZEKA HADI ASILIMIA 4.9

**Jedwali Namba 1: Badiliko la Fahirisi za Bei za Taifa kwa Mwezi Septemba, 2022, (2020 = 100)**

| Na. | MAKUNDI MAKUU YA FAHIRISI | Mizania (Weight) | Oktoba, 2021 | Septemba, 2022 | Oktoba, 2022 | Badiliko la mwezi mmoja | Badiliko la miezi 12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Vyakula na Vinywaji Baridi | 28.2 | 103.15 | 111.89 | 112.55 | 0.6 | 9.1 |
| 2 | Vinywaji Vikali na Tumbaku | 1.9 | 102.65 | 103.52 | 103.60 | 0.1 | 0.9 |
| 3 | Mavazi na Viatu | 10.8 | 104.80 | 107.56 | 107.47 | -0.1 | 2.5 |
| 4 | Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo | 15.1 | 104.25 | 107.98 | 108.06 | 0.1 | 3.7 |
| 5 | Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | 7.9 | 103.41 | 107.24 | 107.74 | 0.5 | 4.2 |
| 6 | Afya | 2.5 | 103.26 | 104.63 | 104.59 | 0.0 | 1.3 |
| 7 | Usafiri | 14.1 | 104.05 | 112.28 | 110.37 | -1.7 | 6.1 |
| 8 | Habari na Mawasiliano | 5.4 | 102.02 | 103.16 | 103.26 | 0.1 | 1.2 |
| 9 | Burudani, Michezo na Utamaduni | 1.6 | 102.43 | 104.67 | 104.64 | 0.0 | 2.2 |
| 10 | Huduma za Elimu | 2.0 | 101.16 | 101.89 | 101.90 | 0.0 | 0.7 |
| 11 | Migahawa na Huduma za Malazi | 6.6 | 105.39 | 107.23 | 107.85 | 0.6 | 2.3 |
| 12 | Huduma za Bima na Fedha | 2.1 | 100.31 | 100.54 | 100.10 | -0.4 | -0.2 |
| 13 | Usafi Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko | 2.1 | 103.06 | 105.32 | 105.50 | 0.2 | 2.4 |
| **JUMLA – FAHIRISI BIDHAA ZOTE** | | **100.0** | **103.61** | **108.73** | **108.73** | **0.0** | **4.9** |
| **Makundi Mengine Teule** | | | | | | | |
| 1 | Fahirisi za Msingi (*Core Index*) | 73.9 | 104.44 | 107.89 | 107.57 | -0.3 | 3.0 |
| 2 | Fahirisi Isiyojumuisha Fahirisi za Msingi (*Non-Core Index*) | 26.1 | 101.24 | 111.10 | 112.01 | 0.8 | 10.6 |
| 3 | Fahirisi za Nishati, Mafuta na Bili za Maji | 5.7 | 103.93 | 112.97 | 112.93 | 0.0 | 8.7 |
| 4 | Fahirisi za Huduma | 37.2 | 103.44 | 106.94 | 106.35 | -0.5 | 2.8 |
| 5 | Fahirisi za Bidhaa | 62.8 | 103.71 | 109.79 | 110.14 | 0.3 | 6.2 |
| 6 | Fahirisi za Bidhaa na Huduma za Elimu | 4.1 | 103.11 | 105.06 | 104.90 | -0.1 | 1.7 |
| 7 | Bidhaa zote isipokuwa Bidhaa za Vyakula na Vinywaji Visivyo na Kilevi | 71.8 | 103.79 | 107.49 | 107.23 | -0.2 | 3.3 |

### 2.1 Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa Kipimo cha Mwaka

Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa kipimo cha mwaka unapima kiwango cha kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi. Jedwali Namba 1 linaonesha kuwa, Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa mwaka ulioishia mwezi Oktoba, 2022 umeongezeka hadi asilimia 4.9 kutoka asilimia 4.8 kwa mwaka ulioishia mwezi Septemba, 2022. Hii inamaanisha kuwa, kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia mwezi Oktoba, 2022 imeongezeka ikilinganishwa na kasi iliyokuwepo kwa mwaka ulioishia mwezi Septemba, 2022. Fahirisi za Bei zimeongezeka kutoka 103.61 mwezi Oktoba, 2021 hadi 108.73 mwezi Oktoba, 2022.


### 2.2 Mfumuko wa Bei wa Bidhaa za Vyakula na Vinywaji Baridi

Mfumuko wa Bei wa Bidhaa za Vyakula na Vinywaji Baridi kwa mwaka ulioishia mwezi Oktoba, 2022 umeongezeka hadi asilimia 9.1 kutoka asilimia 8.3 kwa mwaka ulioishia mwezi Septemba, 2022. Kwa upande mwingine, Mfumuko wa Bei ambao haujumuishi Bidhaa za Vyakula na Vinywaji Baridi kwa mwezi Oktoba, 2022 umepungua hadi asilimia 3.3 kutoka asilimia 3.5 ilivyokuwa mwezi Septemba, 2022.

### 2.3 Mfumuko wa Bei wa Fahirisi za Msingi (Core Inflation)

Fahirisi za bei za msingi zinaandaliwa kwa kutojumuisha bidhaa za vyakula zisizochakatwa; nishati na bili za maji. Kutojumuisha bei za bidhaa ambazo zina sifa ya kubadilika mara kwa mara kwenye Fahirisi za bidhaa na huduma zote, hubakiza Fahirisi ambayo ina mwelekeo imara kwa Watunga Sera. Fahirisi za bei za msingi zinakokotolewa kwa kutumia bei za bidhaa na huduma 297 na mchango wa mizania kwenye Fahirisi zote ni asilimia 73.9. Mfumuko wa Bei wa Fahirisi za Msingi (*Core inflation*) kwa mwezi Oktoba, 2022 umepungua hadi asilimia 3.0 kutoka asilimia 3.3 ilivyokuwa kwa mwaka ulioishia mwezi Septemba, 2022.

**Kielelezo Namba 1: Mwenendo wa Fahirisi za Bei za Taifa na Mfumuko wa Bei Kutoka Mwezi Oktoba, 2021 hadi Oktoba, 2022. (2020 = 100)**




Kielelezo Namba 1 kinaonesha kuwa, Fahirisi za Bei zimekuwa na mwenendo imara kutoka mwezi Oktoba, 2021 hadi mwezi Oktoba, 2022. Katika kipindi hicho, Mfumuko wa Bei pia umekuwa na mwenendo imara ambao ulikuwa kati ya asilimia 3.6 mwezi Machi, 2022 na asilimia 4.9 mwezi Oktoba, 2022.

## 3. FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA KATI YA MWEZI SEPTEMBA NA OKTOBA, 2022

Fahirisi za Bei za Taifa kwa mwezi Oktoba ni 108.73 kama ilivyokuwa kwa mwezi Septemba, 2022. Kutobadilika kwa Fahirisi za Bei za mwezi Oktoba, 2022 zikilinganishwa Septemba, 2022 ni matokeo ya kuongezeka na kupungua kwa bei za baadhi ya bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula.

Aidha, baadhi ya bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula zilizoonesha kuongezeka kwa bei in pamoja na: mchele kwa asilimia 4.3, ulezi kwa asilimia 0.6, mahindi kwa asilimia 2.0, unga wa mahindi kwa asilimia 3.2, kuku kwa asilimia 0.7, samaki wabichi kwa asilimia 0.4, dagaa wabichi kwa asilimia 8.9, dagaa wakavu kwa asilimia 1.0, matunda kwa asilimia 0.7, maharage kwa asilimia 3.9, soya kwa asilimia 5.1, choroko kwa asilimia 0.9, gesi kwa asilimia 5.1, kuni kwa asilimia 2.6,

magodoro kwa asilimia 2.3, sabuni ya unga kwa asilimia 4.0 na vyakula kwenye migahawa kwa asilimia 0.7.

Kwa upande mwingine, baadhi ya bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula zilizoonesha kupungua kwa bei ni pamoja na: ngano kwa asilimia 0.6, mafuta ya kupikia kwa asilimia 0.9, karanga kwa asilimia 0.6, mbogamboga kwa asilimia 1.1, viazi mviringo kwa asilimia 5.6, viazi vitamu kwa asilimia 1.6, mihogo mibichi kwa asilimia 1.2, ndizi za kupika kwa asilimia 3.0, saruji kwa asilimia 0.2, mafuta ya taa kwa asilimia 1.1, mkaa kwa asilimia 0.2, dizeli kwa asilimia 2.5 na petrol kwa asilimia 5.8.

**Jedwali Namba 2: Ratiba ya Utangazaji Fahirisi za Bei za Taifa kwa Miezi Ijayo.**

| Fahirisi za Bei za Taifa | Tarehe ya Toleo |
|---|---|
| Novemba, 2022 | 08 Desemba, 2022 |
| Desemba, 2022 | 09 Januari, 2023 |
| Januari, 2023 | 08 Februari, 2023 |

**Kwa mawasiliano zaidi kuhusu mbinu na kanuni za ukokotoaji wa Fahirisi za Bei za Taifa na maelezo yoyote yanayohusiana nazo tafadhali wasiliana na: -**

Mtakwimu Mkuu wa Serikali,
Ofisi ya Taifa ya Takwimu,
Barabara ya Jakaya Kikwete,
S.L.P. 2683,
Dodoma,
TANZANIA.

Simu: +255 26 -2963822,
Nukushi: +255 26 -2963828,
Barua pepe: sg@nbs.go.tz;
Tovuti: www.nbs.go.tz.